7. Kuingilia data kinyume cha sheria.
8. Ujasusi data.
9. Kuingilia mfumo kinyume cha sheria.
10. Kifaa kisicho halali.
11. Kughushi kunakohusiana na masuala ya kompyuta.
12. Udanganyifu unaohusiana na kompyuta.
13. Ponografia za watoto.
14. Ponografia.
15. Makosa yanayohusiana na utambuzi.
16. Kutoa taarifa za uongo.
17. Ubaguzi.
18. Matusi ya kibaguzi.
19. Mauaji ya kimbari.
20. Taarifa zinazotumwa bila ridhaa.
21. Kufichua taarifa za upelelezi.
22. Kuzuia upelelezi.

23. Unyanyasaji kwa kupitia mtandao.
24. Ukiukaji wa haki bunifu.
25. Wakosaji wakuu.
26. Jaribio la kufanya uhalifu.
27. Kula njama ya kutenda kosa.
28. Ulinzi wa miundo mbinu muhimu ya TEHAMA.
29. Uhujumu wa miundo mbinu muhimu ya TEHAMA.

SEHEMU YA TATU
MAMLAKA YA MAHAKAMA

30. Mamlaka ya mahakama.

SEHEMU YA NNE
UPEKUZI NA UKAMATAJI

31. Upekuzi na ukamataji.
32. Utoaji data.
33. Utunzaji data wa dharura.
34. Utoaji na ukusanyaji wa mwenendo wa data.
35. Utoaji na ukusanyaji wa maudhui katika data.
36. Amri ya mahakama.
37. Matumizi ya kifaa cha TEHAMA katika uchunguzi.
38. Usikilizaji wa maombi.

SEHEMU YA TANO
WAJIBU WA WATOA HUDUMA

39. Kutowajibika kufanya ufuatiliaji.
40. Mtoa huduma ya kuingia kwenye mfumo.
41. Mtunza data.
42. Mhifadhi data kwa muda mfupi.
43. Mtoa huduma ya kuunganisha tovuti.
44. Mtoa huduma ya utafutaji wa taarifa.
45. Notisi ya kuondoa.
46. Wajibu mwingine kutoathiriwa na sheria.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

47. Kinga.
48. Utaifishaji mali.
49. Makosa yanayofanywa na kampuni.
50. Kufifilisha kosa.
51. Mamlaka ya kutengeneza kanuni.

TAARIFA

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni umechapishwa pamoja na madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa ya jumla kwa umma.

Dar es Salaam,
3 Februari, 2015

OMBENI Y. SEFUE
Katibu wa Baraza la Mawaziri

MUSWADA
wa

Sheria inayoainisha makosa yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kuweka utaratibu wa upelelezi, ukusanyaji na matumizi ya ushahidi wa kielektroniki na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina na tarehe
ya kuanza
kutumika

1. Sheria hii itaitwa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015. Sheria hii itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataiteua na kuitangaza katika *Gazeti la Serikali*.

Matumizi

2. Isipokuwa kwa kifungu cha 50, Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Tafsiri

3. Katika sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-
“kuingia” kuhusiana na mfumo wa kompyuta maana yake ni kuingia, kutoa maelekezo, kuwasiliana, kuhifadhi data au kupokea data kutoka katika mfumo wa kompyuta au vinginevyo kutumia rasilimali zozote za mfumo wa kompyuta au

- mtandao au chombo cha kuhifadhi data;
- “mtoa njia” maana yake ni mtu anayetoa huduma ya usambazaji wa data za kielektroniki kwa kusambaza taarifa zilizotolewa na au kwa mtumiaji wa huduma katika mtandao wa mawasiliano au anayetoa fursa ya kuingia kwenye kompyuta au mtandao;
- “mhifadhi data ” maana yake ni mtu anayetoa huduma ya uhifadhi wa data za kielektroniki kwa njia inayojiendesha yenyewe, kwa kupitia mtu kati au kwa utunzaji wa taarifa kwa muda mfupi kwa madhumuni ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa kwa watumiaji wengine wa huduma kiufanisi zaidi pale watakapoomba;
- “mtoto” maana yake ni mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane;
- “ponografia za watoto” maana yake ni aina yoyote ya picha na filamu za ngono zinazo ashiria au kumuonesha:
- (a) mtoto akiwa anashiriki kwa uwazi katika matendo ya ngono;
 - (b) mtu anayeonekana kama mtoto akiwa anashiriki kwa uwazi katika matendo ya ngono; au
 - (c) taswira inayoashiria mtoto akiwa anashiriki kwa udhahiri katika matendo ya ngono;
- “mfumo wa kompyuta” maana yake ni kifaa au mchanganyiko wa vifaa, ikijumuisha mtandao, vifaa vya kuingizia na vya kutolea na ambavyo vinaweza kutumika pamoja na majalada yaliyo na programu za kompyuta, maelezo ya kielektroniki, data za kuingizia na data za kutolea zinazotunza data za hesabu za miongo zilizo na mantiki na udhibiti wa utolewaji wa mawasiliano na majukumu mengine;
- “data kompyuta” maana yake ni uwasilishaji wa maelezo, dhana, taarifa au maelekezo katika namna inayofaa kwa ajili ya kuchakata katika mfumo wa kompyuta, ikijumuisha programu inayofaa kwa ajili ya kuwezesha mfumo wa kompyuta kutelekeza kazi fulani;
- “chombo cha utunzaji wa data ” maana yake ni kifaa chochote au kitu ambacho kutoka kwake data kompyuta au taarifa inaweza kuchakata kwenye mfumo wa kompyuta au kutengenezwa ama kwa msaada wa kifaa kingine au kitu au la;
- “kifaa” inajumuisha:
- (a) programu ya kompyuta, namba tambuzi, mianzi laini au *application*;

- (b) sehemu ya mfumo wa kompyuta kama vile grafiki kadi, kadi ya kutunza kumbukumbu, chipu au kichakataji;
- (c) kifaa cha kutunzia kumbukumbu za kompyuta; na
- (d) kifaa cha kuingizia na kutolea taarifa katika kompyuta na mifumo ya kompyuta;

“mawasiliano ya kielektroniki” maana yake ni uhamishaji wa alama, ishara au data kompyuta ya aina yoyote ile iliyotumwa yote au sehemu kwa njia ya waya, redio, elektromagnetiki, picha ya kielektroniki, picha ya mfumo wa optika au aina nyingine ya mfumo inayofanana na hiyo;

“kifaa cha TEHAMA katika uchunguzi” maana yake ni kifaa cha uchunguzi au kifaa kinachojumuisha mianzi laini au mianzi ngumu iliyowekwa kwenye au inayohusiana na mfumo wa kompyuta au sehemu ya mfumo wa kompyuta na inayotumika kutekeleza kazi zinazojumuisha uingiaji kwa siri au ukusanyaji wa taarifa za kiuchunguzi zinazohusiana na matumizi ya kompyuta au mfumo wa kompyuta;

“zuia” kuhusiana na mfumo wa kompyuta inajumuisha-

- (a) kusababisha kuingiliwa kielektromagnetiki kwa mfumo wa kompyuta;
- (b) kuvuruga mfumo wa kompyuta kwa namna yoyote ile; au
- (c) kuingiza, kutuma, kuzorotesha, kufuta, kuvuruga, kubadilisha au kuzuia data kompyuta;

“mtunza data” maana yake ni mtu anayetoa huduma ya kusambaza data kwa kutunza taarifa inayotolewa na mtumiaji wa huduma hiyo;

“kiunganishi tovuti” maana yake ni alama, neno, msemu, sentensi, au taswira iliyo katika tovuti au taarifa kuhusiana na chanzo kingine kinachopelekea au kufunguka kwa tovuti nyingine;

“haki bunifu” maana yake ni haki zinazotokana au zinazohusiana na haki miliki, hati bunifu, alama za biashara, na mambo mengine yanayohusiana nayo;

“kuingilia” kuhusiana na utendaji kazi wa kompyuta inajumuisha upatikanaji, utazamaji, usikilizaji au kunukuu data yoyote ya mawasiliano ya kompyuta au mifumo ya kompyuta kwa njia yoyote ya kielektroniki;

“afisa utekelezaji wa sheria” maana yake ni afisa wa polisi mwenye cheo cha Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, mpelelezi, afisa Usalama wa Taifa mwendesha mashtaka au mtu aliyeidhinishwa chini ya sheria yoyote;

“Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya TEHAMA.

“kuchapisha” maana yake ni usambazaji, uwasilishaji, uwekaji wazi, kubadilishana, uchapishaji, au usambazaji wa aina yoyote ile;

“mali” maana yake ni mali ya aina yoyote, inayogusika au isiyo gusika na inajumusha:

- (a) fedha yoyote inayotumika au isiyotumika katika Jamhuri ya Muungano Tanzania;
- (b) taarifa, ikijumuisha programu, data au nakala zake, zinazoweza kusomwa na binadamu au kwa kompyuta; au
- (c) haki yoyote au maslahi kwenye mali;

“ubaguzi” maana yake ni taarifa za namna yoyote zinazokuza au kuchochea chuki, ubaguzi au vurugu dhidi ya mtu au kundi la watu kwa msingi wa tabaka, rangi, asili, utaifa, kabila au dini;

“mtoa huduma” maana yeke ni mtu au upande unaowezesha mfumo wa taarifa kupatikana kwa mtu-kati.

SEHEMU YA PILI

MASHARTI YANAYOHUSIANA NA MAKOSA NA ADHABU

Kuingia
kinyume cha
sheria

4.-(1) Mtu hataingia au kusababisha kuingiliwa mfumo wa kompyuta kinyume cha sheria na kwa makusudi.

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni tatu au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungu kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Matumizi ya
mfumo wa
kompyuta
kinyume cha

5.-(1) Mtu hatatumia au kuendelea kutumia mfumo wa kompyuta, kinyume cha sheria na kwa makusudi, baada ya kuisha kwa muda ambao aliruhusiwa kutumia mfumo wa kompyuta.

sheria

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni moja au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au vyote.

Kuingilia mawasiliano kinyume cha sheria

6.-(1) Mtu ambaye, kinyume cha sheria na kwa makusudi-

(a) anaingilia kwa kutumia njia ya kiufundi au kwa njia nyingine yoyote:

- (i) mawasiliano yasiyo ya umma kwenda au kutoka au yaliyo ndani ya mfumo wa kompyuta;
- (ii) mawasiliano yasiyo ya umma ya kielektronaniginetiki yakokayo katika mfumo wa kompyuta usio wa umma; au
- (iii) mfumo wa kompyuta usio wa umma ambao umeunganishwa na mfumo mwingine wa kompyuta.

(b) anakwepa hatua za udhibiti zilizoelekezwa kwa ajili ya kukinga kuingiliwa kwa maudhui yaliyomo kwenye mawasiliano yasiyo ya umma.

(2) Mtu atakayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyo pungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Kuingilia data kinyume cha sheria

7.-(1) Mtu ambaye, kinyume cha sheria na kwa makusudi-

(a) anaharibu au anazorotesha data kompyuta;

(b) anafuta data kompyuta;

(c) anabadili data kompyuta;

(d) anaifanya datamkompyuta ipoteze maana, ishindwe kutumika au ikose ufanisi;

(e) anazuia au anaingilia matumizi halali ya data kompyuta;

(f) anazuia au anamuingilia mtu mwingine anayetumia data kompyuta kihalali; au

(g) anamzuia mtu aliyeidhinishwa kutumia data kompyuta,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume na sheria au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote.

(2) Mtu ambaye-

(a) anawasilisha, anafichua au anasambaza data kompyuta, programu ya kompyuta, ishara ya kuingilia au agizwa kwa mtu ambaye hajaidhinishwa;

(b) anapokea data kompyuta ambayo hajaidhinishwa, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika, kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni mbili au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

(3) Mtu ambaye isivyo halali na kwa makusudi anaharibu au anabadili data yoyote ya kompyuta, iwapo data hiyo inatakiwa kutunzwa kisheria au ni ushahidi kwenye shauri lolote chini ya Sheria hii kwa-

(a) kuondoa au kubadilisha data, programu au taarifa nyingine yoyote iliyoko ndani au nje ya mfumo wa kompyuta;

(b) anawasha, anaingiza au anapakua programu ambayo imetengenezwa kwa lengo la kuondoa au kubadilisha data, programu au aina yoyote ya taarifa iliyoko ndani au nje ya mfumo wa kompyuta; au

(c) anatengeneza, anabadilisha au anaharibu namba ya siri, namba binafsi ya utambulisho au namna inayotumika kuingika kwenye mfumo wa kompyuta,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni ishirini au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au vyote.

Ujasusi data
Sura ya 47

8.-(1) Bila kuathiri masharti ya sheria ya Usalama wa Taifa, mtu hataingilia pasipo idhini na kujipatia data kompyuta iliyokingwa dhidi ya kuingiliwa.

(2) Mtu akatayekiuka kifungo kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni ishirini au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au vyote

Kuingilia
mfumo
kinyume cha
sheria

9. Mtu ambaye, kinyume cha sheria na kwa makusudi anazuia au anaingilia-

(a) utendaji kazi wa mfumo wa kompyuta;

(b) matumizi au uendeshaji wa mfumo wa kompyuta,
atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho

ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni mbili au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote

Kifaa kisicho halali

10.-(1) Mtu hatajishughulisha au kumiliki, kinyume cha sheria-

- (a) kifaa ikijumuisha programu ya kompyuta iliyotengenezwa au inayotumiwa kwa madhumuni ya kutenda kosa;
- (b) namba ya siri ya kompyuta, ishara ya kuingilia au data kama hiyo ambayo inaweza kutumika na mtu yoyote kuingilia mfumo wa kompyuta au sehemu yake kwa lengo la kutenda kosa.

(2) Mtu akatayekiuka kifungo kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika, kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote

Kughushi kunakohusiana na masuala ya kompyuta

11.-(1) Mtu hataingiza, hatabadilisha, hatachelewesha, hatasambaza au hatafuta data kompyuta iliyogushiwa kwa lengo la kutaka itumike kwa madhumuni halali, bila kujali kama taarifa hiyo inasomeka au haisomeki.

(2) Mtu akatayekiuka kifungo kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika, kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni ishirini au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au vyote.

Udanganyifu unaohusiana na kompyuta

12.-(1) Mtu hatasababisha kupotea kwa mali ya mtu mwingine-

- (a) kwa kuongeza, kubadilisha, kufuta, kuchelewesha, kusambaza au kuzuia data kompyuta; au
- (b) kwa kuingilia utendaji kazi wa mfumo wa kompyuta, kwa udanganyifu au ya uongo kwa lengo la kujipatia bila haki manufaa ya kiuchumi.

(2) Mtu akatayekiuka kifungo kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika, kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni ishirini au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua

miaka saba au vyote.

Ponografia za
watoto

13.-(1) Mtu yeyote-

- (a) hatachapisha ponografia za watoto kwa kupitia mfumo wa kompyuta; au
- (b) hatawezesha upatikanaji au kuoneshwa kwa ponografia za mtoto kwa kupitia mfumo wa kompyuta.

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni hamsini au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au vyote.

(3) Mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki, pamoja na adhabu nyingine yoyote, anaweza kuamriwa kumlipa fidia mtu ambaye ameathirika na kosa hilo.

Ponografia

14.-(1) Mtu hatachapisha au kusababisha kuchapishwa kwa kupitia katika mfumo wa kompyuta-

- (a) ponografia; au
- (b) ponografia yoyote iliyo ya kiasherati au chafu.

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika, iwapo ni uchapishaji kuhusiana na-

- (a) ponografia, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni ishirini au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au vyote; au
- (b) ponografia iliyo ya kiasherati au chafu, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni thelathini au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi au vyote.

Makosa
yanayohusiana
na utambuzi

15.-(1) Mtu hatajifanya kuwa mtu mwingine kwa kutumia mfumo wa kompyuta.

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni tano au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au vyote.

Kutoa taarifa za

16. Mtu yeyote anayetoa taarifa, data au maelezo kwa njia ya picha,

- uongo maandishi, alama au aina nyingine yoyote kwenye mfumo wa kompyuta, endapo taarifa, data, au maelezo hayo ni ya uongo, yanapotosha au yasiyo sahihi, atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kutumikia adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita au vyote.
- Ubaguzi **17.**-(1) Mtu, kwa kutumia mfumo wa kompyuta-
(a) hatazalisha vitu vya kibaguzi kwa madhumuni ya kuvisambaza;
(b) hatatoa au kuwezesha kupatikana vitu vya kibaguzi ; au
(c) hatarusha vitu vya kibaguzi.
(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni tatu au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.
- Matusi ya kibaguzi **18.**-(1) Mtu hatamdhihaki mtu mwingine kwa kupitia mfumo wa kompyuta, kutokana na sababu kuwa mtu huyo mwingine ni mmoja kati ya kundi linalotambulika kwa tabaka, rangi, asili, utaifa, kabila au dini fulani.
(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.
- Mauaji ya kimbari **19.**-(1) Mtu hatachapisha au kusababisha kuchapishwa vitu vinavyochochea, kanusha, punguza au halalisha matendo yanayopelekea mauaji ya kimbari na makosa dhidi ya binadamu kwa kupitia mfumo wa kompyuta.
(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi cha kisichopungua miaka mitatu au vyote.
- Taarifa zinazotumwa bila ridhaa **20.**-(1) Mtu-
(a) hataanzisha usambazaji wa taarifa zinazotumwa bila ridhaa;
(b) hatarusha tena au kusambaza upya taarifa zinazotumwa bila ridhaa;
(c) hataghushi taarifa za utambulisho na kuzituma bila ridhaa
(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya kiwango kisichopungua shilingi milioni tatu au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja

au vyote.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “taarifa zinazotumwa bila ridhaa” maana yake ni taarifa au data za kielektroniki amabazo hazijaombwa na mpokeaji.

Kufichua
taarifa za
upelelezi

21.-(1) Mtoa huduma anayepokea amri kuhusiana na upelelezi wa kijinai, inayohitaji usiri, hatatoa taarifa yoyote iliyopo kwenye amri hiyo isivyo halali na makusudi.

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungu kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote.

Kuzuia
upelelezi

22. Mtu ambaye kwa makusudi na kinyume cha sheria ataharibu, atafuta, ataondoa, ataficha, atabadilisha au ataifanya data kompyuta kukosa maana kwa lengo la kuharibu ushahidi au kuchelewesha upelelezi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiwango kisichopungua milioni tatu au kutumikia kifungu kwa muda usiopungua mwaka mmoja au vyote.

(2) Mtu ambaye kwa makusudi atazuia utekeleza au atashindwa kutekeleza amri iliyotolewa na sheria hii, atakuwa ametenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kutumikia kifungu kwa kipindi cha kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Unyanyasaji
kwa kupitia
mtandao

23.-(1) Mtu hataanzisha au kukadimisha mawasiliano yoyote ya kielektroniki kwenda kwa mtu yoyote kwa kutumia mfumo wa kompyuta, kwa lengo la kurubuni, kulazimisha, kutisha au kunyanyasa au kusababisha maudhi ya hisia.

(2) Mtu akataye kiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kutumikia kifungu kwa kipindi cha kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Ukiukaji wa
haki bunifu

24.-(1) Mtu hatatumia mfumo wa kompyuta kwa lengo la kukiuka haki bunifu zinazolindwa na Sheria nyingine yoyote.

(2) Mtu akatayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika iwapo ukiukaji -

(a) hauhusiani na masuala ya kibiashara, kulipa faini isiyo pungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungu kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote;

(b) unagusa masuala ya kibiashara, kulipa faini isiyo pungua shilingi milioni

ishirini au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au vyote.

Wakosaji
wakuu

25.-(1) Mtu yeyote ambaye-

- (a) anafanya kitendo au anaacha kufanya kitendo ambacho kiasi kwamba kutokutenda huko kunasababisha kutendeka kwa kosa;
- (b) anafanya au anaacha kufanya kitendo kwa madhumuni ya kumuwezesha au kumsaidia mtu mwingine kutenda kosa;
- (c) anamsaidia na kumuwezesha mtu mwingine kutenda kosa;
- (d) anamshawishi au kumlipa mtu mwingine kufanya kosa hilo, atachukuliwa kuwa ametenda kosa na atashitakiwa kama mtu aliyetenda kosa.

(2) Mtu anayemlipa mtu mwingine kufanya au kutokufanya kitendo kwa kiasi ambapo, iwapo yeye mwenyewe angefanya kitendo hicho au kutokutenda huko, kitendo hicho kingepelekea kosa kufanyika kwa upande wake na atakuwa na hatia kwa kosa la aina hiyo na atawajibika kwa adhabu sawa kana kwamba yeye mwenyewe angefanya kitendo hicho au kutokutenda huko.

Jaribio la
kufanya uhalifu

26.-(1) Pale ambapo mtu anayekusudia kutenda kosa anaanza kutekeleza kusudio lake na anadhihirisha kusudio lake kwa kitendo kinachoashiria kosa, isipokuwa hatekelezi kusudio lake kwa kiasi cha kutenda kosa hilo, atachukuliwa kuwa ametenda kosa hilo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki-

(a) isipokuwa kwa kiasi cha adhabu haitajalisha iwapo-

- (i) mkosaji anatenda yote ambayo ni muhimu kwa utendaji wa kosa; au
- (ii) utekelezaji wa kusudio lake kwa ukamilifu unazuiliwa na mazingira ambayo hayaingiliani na kusudio lake; au
- (iii) anaacha kutekeleza kusudio lake kwa hiari yake mwenyewe;

(b) kutokana na sababu za mazingira yasiyojulikana kwa mhalifu haiwezekani kutenda kosa.

(3) Mtu yeyote anayejaribu kutenda kosa chini ya sheria hii atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au vyote.

Kula njama ya
kutenda kosa

27. Mtu anayekula njama na mtu mwingine kutenda kosa chini ya Sheria hii, anatenda kosa na iwapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi

milioni moja au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Ulinzi wa
miundo mbinu
muhimu ya
TEHAMA

28.-(1) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali* kuainisha mifumo ya kompyuta kama miundombinu muhimu.

(2) Amri iliyorejewa chini ya kifungo kidogo cha (1) inaweza kuainisha vigezo, miongozo na taratibu kuhusiana na-

- (a) usajili, ulinzi au utunzaji;
- (b) usimamizi wa jumla;
- (c) kuingia, kuhamisha na kudhibiti data;
- (d) kuhakikisha uwepo wa audilifu au uhalali wa data au taarifa;
- (e) njia zitakazotumika kuhifadhi au kutunza data;
- (f) mipango ya kudhibiti majanga iwapo kutatokea uharibifu;
- (g) namna na utaratibu wa kuendesha ukaguzi;
- (h) jambo jingine lolote ambalo ni muhimu kwa ulinzi, usimamizi na udhibiti wa data na rasimali nyingine.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, miundombinu muhimu ya TEHAMA inajumuisha mali, vifaa, mifumo ya kompyuta au mitandao inayoshikika na isiyoshikika ambayo ina umuhimu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi kwamba kutokufanya kazi kwake kuna madhara ya kiusalama, kiuchumi na kijamii.

Uhujumu wa
miundombinu
muhimu wa
TEHAMA

29. Pale ambapo mtu anatenda kosa chini ya sheria hii au sheria nyingine yoyote linalohusiana na miundombinu muhimu, mtu huyo atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia moja au mara tatu ya hasara aliyoisababisha au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote.

SEHEMU YA TATU MAMLAKA YA MAHAKAMA

Mamlaka ya
mahakama

30.-(1) Mahakama zitakuwa na uwezo wa kusikiliza shauri lolote chini ya Sheria hii pale ambapo kosa au sehemu ya kosa -

- (a) limetendeka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (b) limetendeka kwenye meli au ndege iliyosajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (c) limetendwa na mtanzania; au
- (d) limetendwa na mtanzania anayeishi nje Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

- endapo kitendo alichokitenda mtu huyo kingekuwa ni kosa chini ya sheria ya nchi hiyo;
- (e) limetendwa na mtu yeyote, bila kujali utaifa au ukaazi wake au eneo husika, iwapo kosa limefanyika-
- (i) kwa kutumia mfumo wa kompyuta, kifaa au data zilizoko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; au
 - (ii) dhidi ya mfumo wa kompyuta, kifaa au data au mtu aliye ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- (2) Katika kifungu hiki, neno “mahakama” lina maana ya mahakama yenye mamlaka.

**SEHEMU YA NNE
UPEKUZI NA UKAMATAJI**

Upekuzi na
ukamataji

- 31.**-(1) Askari Polisi mkuu wa kituo au afisa utekelezaji wa sheria mwenye cheo cha askari mkuu wa kituo, baada ya kuridhika kuwa kuna sababu za msingi kushuku au kuamini kuwa mfumo wa kompyuta-
- (a) unaweza kutumika kuthibitisha kosa;
 - (b) unachukuliwa na mtu yeyote kutokana na kosa,
- kutoa hati ya upekuzi itakayo muidhinisha afisa utekelezaji wa sheria -
- (i) kuingia kwenye eneo kwa lengo la kupekua au kukamata kifaa au mfumo wa kompyuta;
 - (ii) kuiwekea ulinzi data iliyopatikana;
 - (iii) kuongeza wigo wa upekuzi au uwezo wa kuingia kwenye mfumo mwingine iwapo afisa utekelezaji wa sheria anayefanya upekuzi anazo sababu za kuaminika kuwa data inayotafutwa, inatunzwa kwenye mfumo mwingine wa kompyuta au sehemu yake.
- (2) Upekuzi chini ya kifungu hiki utafanyika kwa mujibu wa sheria zinazo simamia masuala ya upekuzi na ukamataji wa mali.
- (3) Iwapo kifaa au mfumo wa kompyuta umeondolewa au hauingiliki kutokana na upekuzi au ukamataji wa mali, afisa utekelezaji wa sheria, wakati wa upekuzi na ukamataji wa mali -
- (a) ataandaa orodha ya vitu vyote vilivyokamatwa au kufanywa visiingilike, ikijumuisha muda ambao mali ilikamatwa;
 - (b) atampatia nakala ya orodha ya mali iliyokamatwa mtu anayemiliki au mwangalizi wa mfumo husika wa kompyuta.

(4) Mtu anayemiliki au mwangalizi wa mfumo wa kompyuta anaweza kumuomba afisa utekelezaji wa sheria ruhusa ya kuingia au kudurufu taarifa zilizopo kwenye mfumo wa kompyuta baada ya ukamataji wa mali.

(5) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (4), afisa utekelezaji wa sheria anaweza kukataa kuruhusu kuingia kwenye mfumo au kudurufu taarifa iwapo anazo sababu za msingi za kuamini kuwa kuruhusu kuingia au kudurufu taarifa-

(a) itakuwa ni kosa; au

(b) kutaathiri-

(i) uchunguzi unaohusiana na upekuzi

(ii) upelelezi mwingine unaoendelea; au

(iii) shauri lolote lililopo mahakamani au ambalo linaweza kufunguliwa kuhusiana na uchunguzi huo.

(6) Katika kifungu hiki “eneo” inajumuisha ardhi, majengo au chombo cha usafiri.

Utoaji data

32.-(1) Pale ambapo data inanitajika kuwekwa wazi kwa madhumuni ya uchunguzi wa kijinai au kuendeshwa kwa kesi mahakamani, Askari Polisi Mkuu wa kituo au afisa mtekelezaji wa sheria mwenye cheo cha askari mkuu wa kituo anaweza kutoa amri kumtaka-

(a) mtu yeyote kuwasilisha data iliyoainishwa ambayo mtu huyo anaimiliki au iliyo chini ya uangalizi wake ambayo imehifadhiwa kwenye mfumo wa kompyuta; au

(b) mtoa huduma yeyote, kuwasilisha taarifa kuhusiana na mteja zilizo kwenye umiliki au uangalizi wake.

(2) Iwapo kitu chochote kinachohusiana na upelelezi kinajumuisha data iliyohifadhiwa kwenye mfumo wa kompyuta au kwenye kifaa, amri itachukuliwa kumtaka mtu kutoa au kuruhusu upatikanaji wa data hiyo katika namna ambayo inasomeka na inayoweza kuondolewa.

Utunzaji data
wa dharura

33. Pale ambapo Askari Polisi Mkuu wa kituo au afisa utekelezaji wa sheria anazo sababu za kuamini kuwa data kompyuta ambayo inahitajika kwa madhumuni ya uchunguzi inaweza kupotea au kubadilishwa, anaweza kutoa amri itakayomtaka mtu mwenye uangalizi au umiliki wa kifaa au data kompyuta kuitunza kwa kipindi kisichozidi siku kumi na nne.

Utoaji na

34.-(1) Pale Askari Polisi Mkuu wa kituo au afisa mtekelezaji wa sheria

ukusanyaji wa data nyendo

mwenye cheo cha askari mkuu wa kituo anaridhika kuwa data kompyuta inahitajika kwa madhumuni ya uchunguzi, afisa huyo anaweza kutoa amri kwa maandishi kwa ajili ya-

- (a) ukusanyaji au kuweka kumbukumbu za taarifa za kompyuta zinazohusiana na mawasiliano maalum kwa kipindi maalum; au
- (b) kumruhusu na kumsaidia afisa utekelezaji wa sheria kukusanya na kuweka kumbukumbu za data hizo.
- (2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki “data nyendo” maana yake ni taarifa:
 - (a) inayohusiana na mawasiliano kwa mfumo wa kompyuta;
 - (b) iliyotolewa na mfumo wa kompyuta ambao ni sehemu ya mlolongo wa mawasiliano; na
 - (c) inayoonesha chanzo cha mawasiliano, njia iliyotumika, muda, ukubwa, uelekeo na aina ya huduma zinazoambatana nazo.

Utoaji na ukusanyaji wa maudhui katika data

35. Pale ambapo Askari Polisi Mkuu wa kituo au afisa mtekelezaji wa sheria mwenye cheo cha askari mkuu wa kituo anazo sababu za msingi za kushuku au kuamini kuwa yaliyomo kwenye mawasiliano ya kielektroniki yanahitajika kwa madhumuni ya uchunguzi, anaweza kutoa amri ya:

- (a) kukusanya, kurekodi, kuruhusu au kuisaidia mamlaka husika kukusanya au kurekodi taarifa zilizomo kwenye inayohusishwa na mawasiliano maalum yaliyotolewa ka njia ya mfumo wa kompyuta; au
- (b) kumuidhinisha afisa utekelezaji wa sheria kukusanya au kurekodi data kwa kupitia njia ya kiufundi.

Amri ya mahakama

36. Pale ambapo utoaji data au utunzaji data wa dharura chini ya vifungu vya 31, 32, 33, 34 au 35 kwa kadri itakavyokuwa, hauwezi kufanyika bila kutumia nguvu au kutokana na pingamizi kutoka kwa mtu mwenye kumiliki data au thamani ya ushahidi katika data inaweza kuhifadhiwa kwa amri ya mahakama, afisa mtekelezaji wa sheria anaweza kuomba mahakamani amri ya utoaji au utunzaji wa data.

Matumizi ya kifaa cha TEHAMA katika uchunguzi

37.-(1) Pale ambapo afisa utekelezaji wa sheria anaridhika kuwa ushahidi wa msingi hauwezi kukusanywa kwa kutumia utaratibu uliainishwa chini ya Sehemu hii, afisa utekelezaji huyo anaweza kuiomba mahakama kutoa amri ya kuidhinisha matumizi ya kifaa cha uchunguzi.

- (2) Maombi yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) yatajumuisha-
 - (a) jina na anuani ya mtuhumiwa;
 - (b) maelezo ya mfumo wa kompyuta unaolengwa; na

- (c) maelezo ya hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa, madhumuni, kiasi na muda wa matumizi unaokusudiwa.
- (3) Afisa utekelezaji wa sheria atahakikisha kuwa mabadiliko yaliyofanywa kwenye mfumo wa kompyuta au data iliyomo kwenye kompyuta kuhusiana na mtuhumiwa zinajikita kwenye marekebisho yaliyo ya msingi kwa ajili ya uchunguzi na kwamba mabadiliko yanafanywa baada ya kukamilika kwa uchunguzi.
- (4) Wakati wa uchunguzi, afisa utekelezaji wa sheria ataingiza:
- (a) mbinu za kiufundi zilizotuimika, muda na terehe ya maombi;
- (b) utambuzi wa mfumo wa kompyuta na maelezo ya mabadiliko yaliyofanyika wakati wa uchunguzi;
- (c) taarifa yoyote iliyopatikana;
- (5) Taarifa iliyopatikana italindwa dhidi ya mabadiliko, kufutwa bila ya idhini na kuigia kwenye mfumo bila idhini.
- (6) Idhini iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa halali kwa kipindi cha siku kumi na nne.
- (7) Mahakama inaweza, kufuatia maombi, kuongeza muda uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (6) kwa kipindi kingine cha siku kumi na nne au kwa kipindi kingine kwa kadri itakavyoona inafaa.
- (8) Iwapo mchakato wa uwekaji wa kifaa unahitaji kutembelea eneo, masharti ya kifungu cha 30 yatatumika.
- (9) Pamoja na amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), mahakama inaweza, kufuatia maombi, kumuamuru mtoa huduma awezeshe mchakato wa kuweka kifaa.
- (10) Waziri anaweza, kwa Taarifa itakayochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, kuainisha makosa chini ya Sheria hii ambayo mahakama inaweza kutoa amri ya kutumia kifaa cha TEHAMA katika uchunguzi.

Usikilizaji wa maombi

38. Utaratibu wa kusikiliza maombi chini ya Sehemu hii utafanywa kwa upande mmoja na kwa siri.

SEHEMU YA TANO WAJIBU WA MTOA HUDUMA

Kutowajibika kufanya ufuatiliaji

- 39.**-(1) Wakati wa kutoa huduma chini ya Sehemu hii, mtoa huduma-
- (a) hata wajibika kufuatilia data ambayo anaisambaza au kuhifadhi;
- (b) tafuta maelezo au mazingira yanayoashiria shughuli zinazofanywa

kinyume na sheria.

(2) Waziri anaweza kuweka masharti kuhusiana na utaratibu wa watoa huduma kwa jili ya-

(a) kutoa taarifa kwa mamlaka husika ya umma kuhusiana na shughuli zilizo kinyume na sheria zinazofanywa au taarifa inayotolewa na watumiaji wa huduma zao;

(b) kuzipatia mamlaka husika taarifa zitakazoweza kuwatambua watumia huduma, baada ya maombi.

(3) Mtoa huduma hatawajibika kwa uwekaji wazi wa data iliyotolewa kihalali kwa mtu wa tatu baada ya kuthibitisha kwamba:

(a) mtu huyo wa tatu alitenda hivyo pasipo mtoa huduma ya mtandao kufahamu; au

(b) mtoa huduma alitekeleza wajibu unaostahili na alitumia ujuzi ili kuzuia uwekwaji wazi wa data hizo.

(4) Pale ambapo mtoa huduma atakuwa na uelewa juu ya taarifa au kitendo cha kihalifu kwenye mfumo wa kompyuta ambao upo chini ya udhibiti wake, atatakiwa-

(a) kuondoa taarifa juu ya kitendo hicho;

(b) kusimamisha au kusitisha huduma;

(c) kutaarifu mamlaka husika juu ya kitendo au taarifa hiyo, maelezo na utambuzi wa muhusika anayepewa huduma.

Mtoa huduma
ya kuingia
kwenye mfumo

40.-(1) Mtoa huduma ya uwezo wa kuingia kwenye mfumo hatawajibika kwa kurusha au kuendesha mfumo wa kompyuta kwa ajili ya mtu mwingine ikiwa yeye ni mtoa huduma tu ya kuwezesha kuingia kwenye mfumo wa kompyuta au kuendesha vifaa kupitia mfumo wa kompyuta ulio chini ya mamlaka yake kwa masharti kwamba mtoa huduma:

(a) haanzishi urushaji mawasiliano;

(b) hachagui mpokeaji wa mawasiliano; au

(c) hachagui au habadilishi data iliyoko kwenye mawasiliano.

(2) Mawasiliano na masharti ya uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa kompyuta yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) yatajumuisha, utunzaji wa taarifa iliyosambazwa kwa madhumuni ya kuendeleza mawasiliano kwenye mfumo wa kompyuta kwa njia inayojiendesha yenyewe kwa kupitia mtu kati na kwa muda kwa kuzingatia kwamba mawasiliano yanafanyika kwa-

(a) madhumuni ya kuendesha na kusambaza taarifa katika mfumo wa

kompyuta;

- (b) namna ambayo kwa kawaida haiwezi kupatikana isipokuwa tu kwa mpokeaji mlengwa;
- (c) muda ambao sio mrefu sana zaidi ya muda unaofaa kuuwasilisha ujumbe husika kwa mlengwa.

Mtunza Data

41.-(1) Mtunza Data hatawajibika kuhusiana na taarifa zilizohifadhiwa kwa maombi ya mtumiaji wa huduma hiyo, kwa masharti kwamba-

- (a) anaondoa au kusitisha upatikanaji wa taarifa baada ya kupokea amri kutoka taasisi yenye mamlaka au mahakama ya kuondoa taarifa zilizo kinyume cha sheria;
 - (b) baada ya kufahamu kuwa taarifa iliyohifadhiwa iko kinyume cha sheria ataitaarifu mara moja taasisi husika.
- (2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika pale ambapo mpokeaji anafanya hivyo chini ya mamlaka ya mtoa huduma.

Mhifadhi data
kwa muda
mfupi

42. Mtoa huduma ya kuhifadhi data hatawajibika kwa ajili ya utunzaji wa taarifa ikiwa-

- (a) habadilishi taarifa;
- (b) anatekeleza masharti ya utoaji wa uwezo wa kuingia kwenye mfumo;
- (c) anatekeleza kanuni kuhusiana na uboreshaji wa taarifa zilizoainishwa katika namna inayotambulika na walio wengi na kutumika kwenye soko;
- (d) haiingiliani na matumizi halali ya teknolojia inayotambulika na wengi na ianyotumika sokoni kwa ajili ya data kwa ajili ya matumizi ya taarifa hiyo; na
- (e) anachukua hatua za haraka kuondoa au kusitisha matumizi ya/kufikiwa kwa taarifa ambayo imetunzwa baada ya kupokea taarifa kamili kwamba taarifa iliyo kwenye chanzo cha mawasiliano imeondolewa kutoka kwenye mtandao au ufikiwaji wake umesitishwa/ matumizi yake yamesitishwa au kwamba mahakama au mamlaka husika imeamuru itolewe au isitishwe.

Mtoa huduma
ya
kuunganisha
tovuti

43. Mtoa huduma ya kuunganisha tovuti hatawajibika kwa taarifa aliyounganisha iwapo-

- (a) haraka iwezekanavyo anaondoa au anasitisha matumizi ya taarifa baada ya kupokea amri kutoka kwa mamlaka husika ya kuondoa kiunganishi hicho; na

- (b) baada ya kupata uelewa kuhusiana na taarifa zilizo kinyume na sheria kwa namna nyingine zaidi ya amri ya mamlaka ya umma, haraka iwezekanavyo ataitaarifu mamlaka husika.

Mtoa huduma
ya utafutaji wa
taarifa

44.-(1) Mtoa huduma ya utafutaji wa taarifa hatawajibika kwa matokeo ya utafutaji huo, kwa masharti kwamba-

- (a) haanzishi mawasiliano;
- (b) hachagui mpokeaji wa mwasiliano; na
- (c) hachagui au kubadilisha taarifa iliyoko kwenye mawasiliano.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “mtoa huduma ya utafutaji wa taarifa” maana yake ni mtu anayetengeneza au anayeendesha huduma ambayo inatafuta taarifa inayotengeneza kiashiria inayohusiana na taarifa za mtandao au anawezesha upatikanaji wa vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya utafutaji wa taarifa inayotolewa na mtu mwingine.

Notisi ya
kuondoa

45.-(1) Mtu anaweza, kupitia notisi ya kuondoa kumtaarifu mtoa huduma-

- (a) kuhusiana na data au taarifa iliyomnyima mpokeaji au mtu wa tatu haki ya huduma;
- (b) vitu au shughuli ambayo ni kinyume cha sheria; au
- (c) suala lolote linalotekelezwa au linalotolewa kinyume cha sheria hii au sheria nyingine.

(2) Kwa madhumuni ya sehemu hii, notisi ya kuondoa itakuwa katika hali ya kudumu ikitumwa na mlalamikaji kwenda kwa mtoa huduma au wakala wake na itajumuisha-

- (a) jina kamili na anuani ya mlalamikaji;
- (b) saina ya mlalamikaji;
- (c) maelezo ya haki inayodaiwa kuvunjwa;
- (d) maelezo juu ya shughuli ambayo inadaiwa kuwa chimbuko la kitendo kilicho kinyume cha sheria;
- (e) hatua ya utatuzi inayotakiwa kuchukuliwa na mtoa huduma kuhusiana na lalamiko;
- (f) maelezo kuwa mlalamikaji anatenda kwa nia njema;
- (g) maelezo ya mlalamikaji kuwa, kwa ufahamu wake, taarifa iliyomo kwenye taarifa zilizochukuliwa ni sahihi.

(3) Mtu anayewasilisha taarifa kwa mtoa huduma kuhusiana na muamala usio

halali, huku akijua kuwa taarifa hiyo ni potofu, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atatakiwa kulipa faini ya shilingi million tano au kifungo cha mwaka mmoja au vyote.

(4) Mtoa huduma hatawajibika kwa kuondoa taarifa ikiwa ameifanya kwa mujibu wa sheria hii.

Wajibu
mwingine
kutoadhiriwa
na sheria

46. Sehemu hii haitaathiri wajibu wa mtoa huduma:

- (a) uliotolewa na makubaliano;
- (b) ambaye anatenda kwa namna hiyo chini ya kibali au mfumo wa usimamizi uliotajwa chini ya sheria yoyote;
- (c) uliotolewa na sheria au amri ya mahakama ili kutoa, kuzuia au kukataza uingiwaji kwenye mawasiliano ya kieletroniki au kusitisha au kuzuia kitendo kisicho cha halali.

**SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA**

Kinga

47.-(1) Bila kujali sheria nyingine yoyote kinyume na haya, jambo au kitu chochote kitakachofanywa na afisa utekelezaji wa sheria, katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii, hakitampelekea afisa utekelezaji wa sheria kuwajibika moja kwa moja.

(2) Mtu hatawajibika kuhusiana na utekelezaji wa kitendo chochote au kutokutenda, iwapo kitendo hicho au kutokutenda huko kulifanywa kwa nia njema na siyo kwa uzembe, kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Utaifishaji
mali

48.-(1) Pamoja na adhabu iliyotolewa chini ya Sheria hii, mahakama inaweza kutoa amri kwa ajili ya utafishaji wa-

- (a) mali yoyote inayoonekana kuwa ni sehemu ya mapato yatokanayo na kosa; na
- (b) chombo chochote au mali iliyotumika au inayokusudiwa kutumika kutenda au kufanikisha utendaji wa kosa.

(2) Pamoja na amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), mahakama inaweza kumuamuru mtu aliyetiwa hatiani kumlipa fidia mtu aliyeathirika na kosa hilo kwa kadri ambavyo mahakama itaona inafaa.

(3) Mtu aliyetiwa hatiani kwa kosa lililofanywa chini ya Sheria hii atawasilisha hati yake ya kusafiria kwa mamlaka husika hadi hapo atakapolipa faini

au kutumikia kifungo alichohukumiwa kutumikia.

(4) Bila kujali kifungu kidogo cha (3), mahakama inaweza, kufuatia kuwasilishwa kwa maombi na kwa sababu za msingi, kutoa amri ya kuachiliwa kwa hati za kusafiria za mshitakiwa.

Makosa
yanayofanywa
na kampuni

49.-(1) Iwapo kampuni inatiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria hii, mtu yeyote ambaye wakati wa utendaji wa kosa-

- (a) alikuwa ni Mkurugenzi, afisa au vinginevyo anahusika na mambo ya utawala wa kampuni hiyo;
- (b) huku akiwa anajua, aliruhusu kitendo kilichopelekea kosa hilo, atachukuliwa kuwa ametenda kosa hilo na anaweza kushitakiwa na kuadhibiwa ipasavyo.

Kufilisha
kosa

50.-(1) Bila kuathiri sheria nyingine inayotumika Tanzania Bara, Mkurugenzi wa Mashtaka, muda wowote kabla ya mwenendo wa mahakama kuanza na kwa kuzingatia tamko la kukiri kosa kwa hiari la mshitakiwa anaweza kufilisha kosa na kuamuru mtu huyo alipe kiasi cha pesa atakachokitaja ambacho hakitazidi kiasi cha faini kwa kosa hilo.

- (2) Amri ya kufilisha kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa -
 - (a) ya maandishi, ikiainisha kosa lililotendeka, kiasi cha fedha zitakazolipwa na tarehe ya kufanya malipo ikiambatanisha tamko la kukubali kosa lililorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1);
 - (b) ni uamuzi wa mwisho na hautakatiwa rufaa; na
 - (c) na uwezo wa kutekelezwa katika namna sawa na amri ya Mahakama Kuu.

Mamlaka ya
kutengeneza
Kanuni

51. Waziri anaweza kutunga Kanuni kuhusiana na jambo lolote ambalo linatakiwa kuainishwa na Sheria hii au ambalo ni la umuhimu au uharaka kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Muswada huu ni kutunga sheria ambayo itaainisha makosa yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kuweka utaratibu wa upelelezi, ukusanyaji na matumizi ya ushahidi wa kielektroniki.

Muswada unaopendekezwa umegawanyika katika Sehemu Saba.

Sehemu ya Kwanza, inaainisha masharti ya awali, ikiwa ni pamoja na jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada huu.

Sehemu ya Pili, inaainisha makosa na adhabu dhidi ya makosa hayo ndani ya sheria hii.

Sehemu ya Tatu, inatoa mamlaka ya mahakama katika kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusu makosa ya uhalifu wa mtandao yaliyoainishwa katika sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Nne, inaainisha utaratibu juu ya upekuzi na ukamataji wa vifaa vyenye taarifa zinazohitajika kwa ajili ya upelelezi.

Sehemu ya Tano, inaainisha wajibu wa watoa huduma za mtandao wakati wa kutoa huduma hizo.

Sehemu ya Sita, inaweka masharti ya jumla ikiwa ni pamoja na kinga kwa maafisa utekelezaji wa sheria, utafishaji wa mali zinazohusiana na makosa ya mtandao, ufifilishaji wa makosa na uwajibikaji kwa makosa yanayofanywa na kampuni.

Aidha, sehemu hii imeainisha mamlaka ya waziri mwenye dhamana ya kutunga kanuni kuhusiana na masuala yanayohusu utekelezaji wa sheria hii.

Dar es Salaam,
2 Februari, 2015

MAKAME M. MBARAWA
Waziri wa Mawasiliano
Sayansi na Teknolojia